

Hatimaye kilio chetu kimesikia!

***Na: Jacqueline Tesha - Mratibu wa
Kanda ya Kaskazini***

Mradi wa Haki katika Misituz Tanzania ambao unamalengo ya kuhimiza uboreshwaji wa utawala na kuongezeka kwa uwajibikaji katika sekta ya misitu. Mradi kwa kupitia mikakati yake ya ufuatiliaji wa utawala wa misitu na hali ya misitu pamoja na tafti, chambuzi na mawasiliano, umeanza kuleta mafanikio makubwa sana hasa kwa wananchi wanaoishi katika tarafa ya Amani wilayani Muheza mkoani Tanga.

Mafanikio haya yametokana na makala iliyoandikwa na waandishi wa habari ambao walitembelea msitu wa Derema mwaka jana mwezi wa saba. Katika mkala hiyo ambayo ilirushwa na kituo cha ITV pamoja kutolewa na gazeti la kiingereza la "the guardian" wananchi waliomba serekali kuishirikisha katika kusimamia msitu wa Derema ambao ulikuwa umeharibiwa na watu wasiokuwa na nia njema kwa uvunaji haramu wa mbao. Wananchi hao walisema wakiacha msitu huo kuharibiwa wao



Mama Bertha Anderson akielezea kuhusu ushirikiano ambao wameanza kuipata toka serikalini katika kuuhifadhi msitu wa Derema

